**East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature**
*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya
Volume-7 | Issue-11 | Nov- 2024 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2024.v07i11.006

OPEN ACCESS

**Review Article**

# Matumizi Ya Lakabu Za Wanafunzi Kama Mkakati Wa Kurahisisha Ufundishaji Na Ujifunzaji Wa Kiswahili Kama Lugha Ya Kigeni Nchini Tanzania

Joyce Henock Nyiti[1*], Dkt Adventina Buberwa[2]
[1]Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Idara ya Elimu Sekondari Meru
[2]Mhadhiri Mwandamizi Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Article History**
**Received:** 03.10.2024
**Accepted:** 07.11.2024
**Published:** 30.11.2024

**Journal homepage:** https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Miongoni mwa sehemu ambazo lakabu hutumika ni katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni (Lgn). Matumizi hayo yameibua maswali kuhusu mchango unaotokana na matumizi ya lakabu katika ufundishaji wa lugha ya kigeni. Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu matumizi ya lakabu katika ufundishaji wa Lgn lakini hakuna utafiti uliochunguza kama matumizi ya lakabu yanachangia kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni. Suala hilo limeacha maswali kuhusu mchango wa matumizi ya lakabu katika kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Lgn. Makala hii imebaini namna lakabu zinavyotumika kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Data hiyo imepatikana kwa kuchunguza ni kwa namna gani lakabu za wanafunzi zinatumiwa kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania. Mbinu za usaili na hojaji zimetumika kukusanya data kutoka kwa walimu 6 wanaofundisha Kiswahili kama Lgn na wanafunzi 12 wanaojifunza lugha hiyo katika Chuo cha Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa (MS TCDC) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Ukusanyaji na uchaganuzi wa data za makala hii umeongozwa na Modeli ya Elimu ya Kijamii ya Robert C. Gardner ya 2005. Mihimili miwili ya modeli hiyo imetumika kufafanua matokeo ya makala hii, kwanza, ni mhimili unaoeleza kuwa mjifunzaji wa lugha ya pili/Lgn mwenye motisha ya kujifunza lugha hiyo hutumia mikakati inayorahisisha ujifunzaji. Pili, ni mhimili unaohusu mtazamo kuhusu mazingira ya ujifunzaji wa lugha ya pili/kigeni kipengele kinachosisitiza kuwa walimu wanaofundisha lugha ya pili/kigeni wanapaswa kuyamudu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Matokeo yameonesha kuwa baadhi ya walimu wanatumia lakabu kurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn kwa namna mbili. Mosi, ni kuwafundisha wanafunzi kulingana na tabia na uwezo unaobainishwa na lakabu zao. Pili ni kutumia lakabu kurahisisha ufundishaji wa vipengele vya sarufi. Pia, matokeo yameonesha kuwa baadhi ya wanafunzi hujifunza Kiswahili kama Lgn kwa kutumia mikakati inayotokana na lakabu zao. Mikakati hiyo ni kusikiliza muziki, kujifunza maneno mapya ya Kiswahili kutokana na lakabu, uandishi wa sentensi zinazohusu lakabu na uandishi wa historia za lakabu. Ili kuongeza idadi ya walimu wenye maarifa hayo, makala hii inapendekeza kuwapa walimu mafunzo kuhusu namna lakabu zinavyoweza kutumika kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn.

**Keywords:** Lakabu, Ufundishaji wa Lugha ya Kigeni (Lgn), Mkakati wa Ufundishaji, Motisha, Mazingira ya Ujifunzaji.

**Copyright © 2024 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.0 UTANGULIZI

Makala hii inahusu namna lakabu za wanafunzi zinavyotumiwa kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni (kuanzia sasa Lgn) katika taasisi zinazofundisha Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania. Lakabu zilizohusishwa katika makala hii ni lakabu za wanafunzi ambazo hupewa au kujipa kabla au baada ya

***Corresponding Author:** Joyce Henock Nyiti
Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Idara ya Elimu Sekondari Meru

kufika Tanzania katika taasisi zinazofundisha Kiswahili kama Lgn. Ili kuweka bayana maarifa yanayohusu namna matumizi ya lakabu za wanafunzi yanavyorahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn, makala hii imefafanua vipengele vifuatavyo: mosi, matumizi ya lakabu katika ufundishaji wa lugha ya kigeni na hali ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania, pili, Modeli ya Elimu ya Kijamii ya Robert C Gardner ya 2005, tatu, methodolojia ya utafiti, na nne, ufafanuzi kuhusu namna lakabu za wanafunzi zinavyotumiwa kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania. Mwisho wa makala hii ni hitimisho linalotoa majumuisho.

**1.1 Matumizi ya Lakabu katika Ufundishaji wa Lugha ya Kigeni**

Lakabu ni istilahi inayotokana na neno la Kiingereza -"*an eke-name*"- lenye maana ya jina jingine (McDowell, 1981; Lakaw, 2006). Maelezo ya wataalamu mbalimbali (Mapako, 2015; Mulokozi, 2017; Masoud, 2018) yanaonesha kuwa kwa miaka mingi lakabu zimetumika katika jamii kama kipengele cha kiutamaduni chenye lengo la kujenga uhusiano miongoni mwa watu, kukosoa na kurekebisha matendo, sifa na tabia za watu zisizokubalika katika jamii. Lakini Afful (2007) anadhihirisha kuwa mawanda ya matumizi ya lakabu yamepanuka na lakabu hizo kutumika katika mazingira mengine yakiwamo mazingira ya kitaaluma. Mtaalamu huyo anafafanua kuwa katika mazingira ya kitaaluma matumizi ya lakabu yameshamiri zaidi ikilinganishwa na mazingira mengine. Pengine hali hiyo inatokana na kauli iliyowahi kutolewa na Kielkiewicz-Janowiak (2000) na Mapunda (2014) kuwa lakabu katika mazingira ya kitaaluma hutumiwa kwa sababu ya kuakisi utendaji, sifa na tabia za wanaopewa lakabu.

Katika kudhihirisha hali hiyo Mapunda (2014), Sobane (2016), Chamo (2019) na Mensa na Ndileme (2020) wameshughulikia matumizi ya lakabu za wahadhiri. Kwa pamoja wamebaini kuwa lakabu hutolewa kwa wahadhiri kwa lengo la kuwapa utambulisho unaoakisi sifa na tabia zao katika mazingira ya kitaaluma. Maelezo zaidi yanatolewa na Mapunda (2014) na Sobane (2016) kuwa baadhi ya lakabu za wahadhiri si tu hutumiwa kama utambulisho wa wahadhiri bali wanafunzi huzitumia kujikumbusha dhana muhimu zilizofundishwa na wahadhiri hao. Maelezo hayo yanaonesha kuwa licha ya lakabu za wahadhiri kuwa ni utambulisho wao bado zina mchango katika ujifunzaji. Hata hivyo, tafiti hizo hazifafanui ni kwa namna gani lakabu zinatumiwa na wanafunzi kujikumbusha dhana zilizofundishwa.

Kwa upande mwingine, wataalamu wengine wamechunguza matumizi ya lakabu za wanafunzi katika vyuo vikuu na shule za sekondari. Wataalamu hao (Afful, 2006; Afful, 2007; Kuranchie, 2012; Starks na wenzake, 2012; Filani na Melefa, 2014; Koehn, 2015; Atolagbe na wenzake, 2015) kwa pamoja wanakubaliana kuwa lakabu hizo hutumika kama utambulisho wa wanafunzi unaoakisi sifa na matendo yao. Lakini, Filani na Melefa (2014) na Atolagbe na wenzake, 2015) wanaongeza matumizi mengine ya lakabu katika mazingira ya kitaaluma kuwa ni kuchochea ubunifu wa matumizi ya lugha. Maelezo hayo yanazidi kudhihirisha umuhimu wa matumizi ya lakabu katika ujifunzaji hususani wa lugha. Hii ni kwa sababu licha ya matumizi ya lakabu hizo kutohusishwa na ufundishaji na ujifunzaji lakini imebainika kuwa matumizi yake yanachochea ubunifu wa matumizi yake katika lugha. Lakini, tafiti hizo hazitoi ufafanuzi kuhusu namna lakabu zinavyochochea ubunifu wa matumizi ya lugha.

Vilevile, tafiti zingine (Diao, 2014; Bobrova, 2022; Xinran, 2023) zimefanyika kuhusu matumizi ya lakabu katika mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa Lgn. Diao (2014) katika utafiti wake uliowahusisha wanafunzi wa Kichina wanaojifunza Kiingereza anaeleza kuwa matumizi ya lakabu huwapa wanafunzi furaha ya kujifunza lugha ya kigeni. Kauli hiyo ameitoa akimakinikia matumizi ya lakabu za kujipa zinazotokana na lugha ya Kiingereza katika ujifunzaji wa lugha hiyo. Hali hiyo ni tofauti na utafiti wa Bobrova (2022) uliofanyika nchini Urusi ambao pia umeshughulikia lakabu zinazotokana na lugha lengwa ambayo ni Kirusi katika ujifunzaji wa lugha hiyo. Utafiti huo umeonesha kuwa walimu walipendekeza lakabu za Kirusi za watu maarufu na wanasiasa ili wanafunzi wazitumie katika ujifunzaji wa Kirusi kama Lgn. Hata hivyo, licha ya lakabu hizo kutokana na lugha lengwa hazikuwasaidia wanafunzi kufanikiwa kupata umilisi wa lugha hiyo jambo lililowasababisha kushindwa kushiriki katika mazungumzo kwa lugha ya Kirusi. Tukiangalia lakabu zilizotumiwa na wanafunzi kujifunza Lgn katika tafiti za Diao na Bobrova zinatokana na lugha lengwa. Lakini pamoja na kauli aliyowahi kuitoa Diao kuwa kujifunza Lgn kwa kutumia lakabu zinazotokana na lugha hiyo hurahisisha ujifunzaji wake hali ilikuwa tofauti katika utafiti wa Bobrova ambapo pamoja na wanafunzi kujifunza Kirusi kwa kutumia lakabu zinazotokana na lugha hiyo hawakufanikiwa kujifunza lugha husika. Kinachoonekana ni kuwa katika tafiti zote wanafunzi wametumia lakabu zinazotokana na lugha ya kigeni waliyojifunza lakini kundi moja la wanafunzi wamefanikiwa kujifunza Lgn kwa kutumia lakabu zilizotokana na lugha husika huku kundi jingine wakishindwa kujifunza lugha lengwa licha ya kutumia lakabu zilizotokana na lugha hiyo. Aidha, hakuna utafiti miongoni mwa tafiti hizo ulioeleza ni kwa namana gani lakabu zinatumika kujifunza lugha ya kigeni. Kutokana na kauli iliyowahi kutolewa na Diao (2014) kuwa matumizi ya lakabu hurahisisha ujifunzaji wa Lgn mtafiti alipata maswali yaliyohitaji majibu yanayotokana na namna lakabu zinavyotumika katika ujifunzaji wa Lgn. Kwa hiyo,makala hii imejadili na kuweka bayana maarifa kuhusu namna lakabu za wanafunzi zinavyotumiwa kama mkakati wa

kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn.

### 1.2 Ufundishaji wa Kiswahili Kama Lugha ya Kigeni Nchini Tanzania

Ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania ulianza katika kipindi cha ukoloni. Wakati huo wakoloni walijifunza Kiswahili kwa ajili ya kuwasiliana na wafanyakazi wa Kitanzania katika shughuli mbalimbali zilizohusishwa na ukoloni. Aidha, kwenye miaka ya 1967 serikali ya Tanzania ilianza kupokea wataalamu wa kujitolea kutoka nchi kama Denmaki ili kufanya kazi za kimaendeleo. Kutokana na hali hiyo, mafunzo ya lugha ya Kiswahili yalianza kutolewa nchini Tanzania ili wafanyakazi hao waweze kukamilisha kazi za kimaendeleo zilizokusudiwa.

Kuanzia miaka ya 1980 kulikuwa na ongezeko la wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni waliofika Tanzania kutoka mataifa kama Denmaki, Marekani, Ufini, Ujerumani na Uingereza. Wengi miongoni mwa wajifunzaji hao walikuwa wanafunzi wa vyuo vikuu kutoka nchi zilizotajwa. Kufika kwa wanafunzi hao Tanzania kulitokana na kuanzishwa kwa programu mbalimbali za ufadhili wa wanafunzi wa vyuo vikuu ili wakajifunze Kiswahili ng'ambo na kukamilisha masomo yao ya digrii (Wa'Njogu, 2008). Hivyo, hali hiyo iliwaruhusu wanafunzi kujifunza Kiswahili wakiwa ndani ya jamii ya wazungumzaji wazawa wa Kiswahili. Ili kutimiza mahitaji ya wajifunzaji hao, mbinu mbalimbali za ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn zimekuwa zikitumika kurahisisha ufundishaji huo. Mathalani, Fatawi (2019) na Saleh (2019) wanaeleza kuwa mkakati binafsi ni mbinu mojawapo inayotumika kufundisha na kujifunza Kiswahili kama Lgn Tanzania. Pia, Makame (2020) amebainisha mbinu mbalimbali zinazotumika kufundisha Kiswahili kama Lgn zikiwapo mbinu za ufundishaji Lgn zinazosisitizwa katika katika mkabala wa kimawasiliano. Vilevile, Said na Chipila (2023) wamebainisha matumizi ya familia wenyeji kama mbinu ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Aidha, wataalamu hao wameeleza namna kila mbinu inavyorahisisha ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn. Hata hivyo, hakuna utafiti ulioshughulikia matumizi ya lakabu katika ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania, hivyo, hali hiyo imeacha nafasi ya uhitaji wa maarifa hayo. Kwa kuwa imebainika kuwa lakabu za wanafunzi hutumika katika taasisi zinazofundisha Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania, makala hii imejadili namna lakabu zinavyotumiwa na walimu na wanafunzi kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn katika vyuo vya MS TCDC na SUZA nchini Tanzania.

## 2.0 Modeli ya Elimu ya Kijamii ya Robert C. Gardner (2005)

Modeli ya Elimu ya Kijamii (MEK) ya Robert C. Gardner (2005) ni sehemu kubwa ya Nadharia ya Motisha ya Ujifunzaji wa Lugha ya Pili/Kigeni. Modeli hiyo imejengwa na mambo mawili yanayohusiana na ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili/kigeni. Mambo hayo ni motisha ya mjifunzaji na uwezo wa mjifunzaji. Kwa mujibu wa Gardner, motisha ya mjifunzaji imejengwa na mtazamo kuhusu mazingira ya ujifunzaji wa lugha ya pili/kigeni, mwingiliano wa tamaduni na matarajio ya kuitumia lugha ya pili/kigeni baadaye. Mihimili hiyo kwa pamoja humrahisishia mjifunzaji wa lugha ya pili/kigeni kupata mafanikio katika ujifunzaji wa lugha. Lakini, ikiwa mihimili hiyo inampa mjifunzaji hofu ya kujifunza, mafanikio ya ujifunzaji huwa ya chini. Kwa upande mwingine, Gardner (2005) anaeleza kuwa mjifunzaji wa Lgn hufanikiwa kujifunza lugha hiyo kutokana na kuwa na uwezo wa kujifunza, kuitumia na kuikumbuka lugha anayojifunza. Kwa kuwa makala hii ilishughulikia matumizi ya lakabu za wanafunzi kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn, mihimili iliyotumiwa kufafanua matokeo ni mtazamo kuhusu mazingira ya ujifunzaji na motisha ya mjifunzaji. Mhimili wa mtazamo kuhusu mazingira ya ujifunzaji umetumiwa kwa sababu miongoni mwa mambo yaliyosisitizwa ni kuwa walimu wanaofundisha lugha ya pili/kigeni wanapaswa kuyamudu mazingira ya ufundishaji wa lugha husika. Pia, mhimili wa motisha ya mjifunzaji umetumika kwa sababu Gardner ameeleza kuwa mjifunzaji mwenye motisha ya kujifunza lugha ya pili/kigeni hutumia mikakati mbalimbali ili afanikiwe kujifunza lugha hiyo.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Data za makala hii zimekusanywa kwa mbinu ya usaili na hojaji kutoka kwa walimu 6 wanaofundisha Kiswahili kama Lgn na wanafunzi 12 wanaojifunza Kiswahili kama Lgn. Mbinu za usampulishaji lengwa, tajwa na usampulishaji kwa kutegemea fursa ya upatikanaji zimetumika kuwapata watoataarifa kutoka katika Chuo cha Maendeleo na Ushirirkiano wa Kimataifa (MS TCDC) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Watoataarifa hao waliteuliwa kwa sababu ya kuhusika moja kwa moja katika matumizi ya lakabu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Hivyo, watoataarifa hao walikuwa na maarifa yaliyohitajika katika makala hii. Aidha, mbinu ya kusimba maudhui ilitumika katika kuchambua namna lakabu zilivyotumika kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Ufafanuzi wa matokeo umetumia mkabala mseto kwa kuongozwa na Modeli ya Elimu ya Kijamii (MEK) ya Robert C. Gardner (2005).

## 4.0 Matumizi ya Lakabu za Wanafunzi kama Mkakati wa Kurahisisha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania

Kama ilivyoelezwa awali katika sehemu iliyotangulia, ni jambo la kawaida wanafunzi kupewa au kujipa lakabu za kutumia wakati wa ufundishaji na

ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn katika taasisi zinazofundisha Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania. Makala hii imebaini kuwa wanafunzi hupewa au hujipa lakabu kabla na baada ya kufika katika taasisi zinazofundisha Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania na lakabu hizo hutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn katika taasisi husika. Makala hii imebaini lakabu 40 ambazo wanafunzi walipewa wazitumie wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn katika taasisi zilizofanyiwa utafiti. Lakabu hizo zimetokana na aina mbalimbali za majina kama vile majina ya watu, wanyama, ndege, mimea, madini na majina ya kawaida. Pia, lakabu hizo zimetokana na lugha mchanganyiko ambazo ni Kiswahili, Kimeru, Kimasai Kizanaki Kiingereza na Kijerumani. Makala hii imebaini kuwa lakabu za wanafunzi zinatumiwa kwa namna mbalimbali katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania. Miongoni mwake ni kutumika na baadhi ya walimu na wanafunzi kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn.

Matumizi ya lakabu kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn yamegawanywa katika sehemu mbili. Kwanza, ni namna lakabu zinavyotumika kurahisisha ufundishaji. Pili, ni namna lakabu zinavyotumika kama mkakati wa kurahisisha ujifunzaji. Matumizi hayo yanafafanuliwa kama ifuatavyo:

### 4.1 Matumizi ya Lakabu katika Kurahisisha Ufundishaji

Makala hii imebaini namna mbalimbali ambazo lakabu hutumiwa na walimu kurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn.

#### 4.1.1 Ufundishaji Kulingana na Tabia na Uwezo wa Wanafunzi Unaobainishwa na Lakabu zao

Ufundishaji wa Lgn unahitaji walimu wenye ubunifu wa kutumia mitindo mipya ya ufundishaji wa lugha ya kigeni (Saleh, 2019). Pia, MEK imesisitiza kuwa ufundishaji wa lugha ya pili/kigeni unahitaji walimu wenye uwezo wa kuyamudu mazingira ya ufundishaji wa Lgn. Wakati wa usaili kuhusu matumizi ya lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn, ilibainika kuwa baadhi ya wanafunzi hupewa lakabu zinazohusishwa na tabia, matarajio na uwezo wao katika ujifunzaji. Baadhi ya walimu hutafsiri lakabu hizo na kuwaweka wanafunzi katika makundi kulingana na tafsiri hizo ili kurahisisha ufundishaji. Kutokana na mahojiano, walimu waliwaweka wanafunzi katika makundi matatu yaliyotokana na tafsiri za lakabu zao.

Kundi la kwanza ni wanafunzi wenye tabia ya kujifunza polepole. Katika majibu yaliyotolewa na watoataarifa, ilibainika kuwa baadhi ya wanafunzi walipewa lakabu kutokana na tabia ya kupenda kujifunza polepole licha ya kuwa na uwezo mkubwa wa ujifunzaji. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wanafikia malengo yao, walipangwa katika darasa la wanafunzi wanaopenda kujifunza polepole. Nukuu ifuatayo inadhihirisha suala hilo:

***Data Na. 1:***

…nilikuwa na mwanafunzi ambaye alitaka kujifunza polepole. Wakati wa kuwapa wanafunzi lakabu alinieleza kuwa hapendi darasa la mchakamchaka yeye anapenda kujifunza polepole, hivyo alijiita *Polepole*….na mimi nilimpanga katika darasa la kujifunza polepole. …pamoja na kujifunza polepole kufikia mwisho wa kozi yao alikuwa ni mmoja kati ya wanafunzi waliofanikiwa kujifunza Kiswahili kwa kiwango cha juu.

Data Na. 1 katika nukuu hiyo inabainisha kundi la wanafunzi waliopenda kujifunza polepole. Kwa kuzingatia hilo, mwalimu aliwapanga wanafunzi wapendao kujifunza polepole kulingana na matashi yao akiwamo mwanafunzi aliyejiita ‘Polepole’ ambaye hatimaye alimaliza kozi hiyo kwa mafanikio makubwa licha ya kujifunza polepole. Pia, walimu walibaini kundi la wanafunzi lililopewa lakabu zilizohusishwa na matarajio yao. Wanafunzi hao waliwekwa katika darasa ambalo lilifundisha kulingana na matarajio ya wanafunzi. Kama inavyoonekana katika nukuu inayofuata, wanafunzi hao walihitaji kuwa na mafanikio ya kiwango cha juu katika ujifunzaji wao wa Kiswahili, kama inavyoonekana katika nukuu inayofuata.

***Data Na. 2:***

…nilikuwa na wanafunzi watatu ambao waliitwa *Kamusi*, *Kasuku* na *Kiswahili*, wanafunzi hao walikuwa na matarajio ya kuwa na mafanikio ya juu katika ujifunzaji wa Kiswahili. Baada ya kufahamu hivyo, niliwapanga katika darasa la wanafunzi wanaojifunza haraka, haraka, haraka. Sisi hapa tunaita darasa la haraka tatu…walifurahi sana…

Data Na. 2 hapo juu inabainisha namna baadhi ya wanafunzi walivyokuwa wamepania kukijua Kiswahili kulingana na matarajio yao. Majina waliyojipatia wanafunzi hao kama *Kamusi*, *Kasuku* na *Kiswahili* yaliakisi matarajio waliyokuwa nayo. Kutokana na lakabu hizo kubainisha matarajio ya wanafunzi, walimu walitambua namna ya kuwapanga wanafunzi katika madarasa kulingana na uwezo wa kujifunza. Taarifa katika nukuu inayofuata zinaonesha kuwa baadhi ya wanafunzi walikuwa na uwezo mkubwa wa kujifunza ilhali wengine walikuwa na uwezo mdogo. Kutokana na tofauti hizo, walimu waliwapanga wanafunzi katika madarasa yaliyoendana na tofauti zao. Katika kuthibitisha hilo, hebu tuangalie Data Na. 3 ifuatayo:

***Data Na. 3:***

…mwaka 2018 nilifundisha darasa ambalo lilikuwa na wanafunzi wenye uwezo tofauti sana wa ujifunzaji na walikuwa na lakabu zinazoonesha tofauti zao za ujifunzaji. Kwa mfano: *Ajuza*, *Konokono*,

*Polepole* na *Sisimizi* walikuwa na ujifunzaji wa polepole. Pia, kulikuwa na wanafunzi wenye uwezo mkubwa wa kujifunza kama *Almasi* na *Zawadi* na wengine… baada ya kufahamu kuwa lakabu zao zilitokana na tofauti zao za uwezo wa ujifunzaji niliwagawa katika madarasa tofauti yanayoendana na uwezo wao. Darasa moja ni la 'haraka' na darasa jingine ni la 'haraka haraka' na darasa la 'haraka, haraka, haraka'… au tunasema darasa la haraka moja, haraka mbili au darasa la haraka tatu… unajua wanafunzi wa kigeni hawapendi kuonekana kuwa wana uwezo mdogo wa ujifunzaji. Hivyo, tunatumia maneno ambayo hayaoneshi kuwanyanyapaa…

Data Na. 3 hapo juu inaonesha kuwa lakabu za wanafunzi zinaweza kubainisha tabia na uwezo wa wanafunzi katika ujifunzaji, hii ndiyo sababu katika Data Na. 3 inabainishwa kwamba walimu waliwapanga wanafunzi katika makundi matatu ya ujifunzaji. Ili kuepuka lugha za unyanyapaa, makundi hayo yaliitwa kundi la 'haraka moja', kundi la 'haraka mbili' na 'kundi la haraka tatu'. Tafsiri yake kutokana na mahojiano ni kwamba, 'haraka moja' ni darasa la wanafunzi wenye uwezo mdogo wa kujifunza. Darasa la 'haraka mbili' ni wanafunzi wenye uwezo mkubwa wa kujifunza lakini darasa la 'haraka tatu' ni la wanafunzi wenye uwezo mkubwa zaidi.

Hivyo basi, wanafunzi kama *Ajuza, Konokono* na *Sisimizi* walipangwa katika darasa la 'haraka moja' kwa sababu walikuwa na uwezo mdogo. Aidha, *Polepole* alipangwa katika darasa la 'haraka mbili' kwa sababu alikuwa na uwezo mkubwa lakini hakutaka kujifunza kwa haraka. Vilevile, *Almasi* na *Zawadi* walipangwa katika darasa la 'haraka tatu' kwa sababu walikuwa na uwezo mkubwa na walipenda kujifunza kwa haraka. Wanafunzi wengine waliopangwa katika darasa la haraka tatu ni *Kamusi, Kasuku* na *Kiswahili* kwa sababu nao walikuwa na uwezo mkubwa na walihitaji kujifunza kwa haraka ili wafikie matarajio ya kuwa wazungumzaji wakubwa wa Kiswahili.

Upangaji wa wanafunzi katika madarasa kutokana na lakabu zao umeonesha kuwa baadhi ya walimu walitumia lakabu za wanafunzi kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn. Aidha, upangaji huo umetumika kwa namna isiyowanyanyapaa wanafunzi. Kwa hiyo, walimu wa namna hiyo kwa mujibu wa MEK wana uwezo wa kuyamudu mazingira ya ufundishaji wa Lgn kwa vile modeli hiyo imesisitiza kuwa mwalimu anayefundisha Lgn anapaswa kuyamudu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Suala la walimu kuweza kubaini tabia na uwezo tofauti wa wanafunzi katika ujifunzaji kutokana na lakabu zao na kuweza kuwagawa wanafunzi katika madarasa yanayoendana na uwezo wao pasipo kuwanyanyapaa, linaonesha uwezo wa kuyamudu mazingira ya ufundishaji wa Lgn. Jambo hilo limedhihirisha ubunifu wa walimu katika matumizi ya lakabu za wanafunzi kama mkakati unaorahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn.

### 4.1.2 Kurahisisha Ufundishaji wa Vipengele vya Sarufi

Mahojiano yaliyofanyika kuhusu matumizi ya lakabu za wanafunzi kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn yalionesha kuwa walimu 03 walitumia lakabu kufundishia sarufi. Zifuatazo ni data zinazothibitisha maelezo hayo:

***Data Na. 4:***

…katika programu moja ya miaka ya hivi karibuni nilikuwa na mwanafunzi aliyeitwa *Norlan Lockhunter*. Baada ya watu kushindwa kutamka jina lake kwa usahihi aliamua kutafsiri jina la baba yake ili apate lakabu ya Kiswahili akajiita 'Mawindo'. Niligundua kuwa kile kipengele cha mwisho cha jina la baba yake ni mwindaji na si mawindo. Hivyo, nilimrekebisha nikamwambia kuwa *hunter* ni 'mwindaji', kwa hiyo mtu anayewinda ni mwindaji. Kwa hiyo, akaitwa *Mwindaji*….mara nyingi ninafundisha wanafunzi wa hatua ya tatu kwa hiyo nimekuwa nikiwapa lakabu zinazoundwa na viambishi mbalimbali na kuwafundisha kazi za viambishi hivyo.

…ninakumbuka baada ya kuchambua kazi za viambishi katika lakabu za baadhi ya wanafunzi, baadaye wanafunzi hao walinipa vitenzi wakitaka tuunde…! Sijui niseme majina yao ya Kiswahili?... na tulifanya hivyo pamoja…

…ninaona kwa sasa katika chuo chetu baadhi ya walimu wanawapa wanafunzi kazi za kuandika kuhusu lakabu zao na kufundisha vipengele mbalimbali vya sarufi vinavyojitokeza katika kazi hizo…

Katika Data Na. 4 imebainika kuwa mtoataarifa mmoja ambaye ni mwalimu ana utaratibu wa kutumia lakabu kufundisha sarufi kwa kufundisha kazi za viambishi vilivyounda lakabu. Hivyo, lakabu zinatumiwa na baadhi ya walimu kama mkakati au mbinu ya kufundisha sarufi.

Makala hii imebaini pia kuwa wapo walimu ambao huwapa wanafunzi kazi za kuandika historia za lakabu zao na kuziwasilisha darasani. Wakati wa uwasilishaji, mwalimu husika hunukuu sarufi mpya na makosa ya kisarufi yanayojitokeza kisha baadaye au siku inayofuata hufundisha sarufi husika. Data Na. 5 ifuatayo inadhihirisha suala hilo:

***Data Na. 5:***

….kwa mfano mwanafunzi wangu aliyekuwa anaitwa *Tausi* nilimpa kazi ya kuandika kuhusu ndege tausi. Ninakumbuka aliandika kazi nzuri lakini sentensi zake zilikuwa na makosa mengi ya kisarufi. Niliyanukuu makosa hayo na kufundisha sarufi yake siku iliyofuata. ….mwanafunzi huyo alikuwa miongoni

wanafunzi waliokuwa wa kwanza kuelewa kwa sababu ndicho kitu kilichokuwa kinamsumbua…kazi hizo zinanisaidia kufundisha sarufi bila hata kufuata mtaala na wanafunzi wanaelewa kwa haraka sana…

Data Na. 5 hapo juu inaonesha kuwa baadhi ya walimu wanapowapa wanafunzi kazi za kandika na kuziwasilisha hunukuu makosa ya kisarufi na kusahihisha makosa waliyoyabaini katika kazi za wanafunzi. Utaratibu huo huwawezesha wanafunzi kuelewa vizuri zaidi sarufi kama ilivyobainishwa katika Data Na. 5 hapo juu kwamba, mwanafunzi aliyeandika kuhusu lakabu yake 'Tausi' alikuwa miongoni mwa wanafunzi wa kwanza kuelewa sarufi baada ya mwalimu kufanya masahihisho.

Aidha, walimu wengine hunukuu sarufi mpya iliyotumiwa na baadhi ya wanafunzi kisha hufundisha sarufi hizo siku inayofuata. Hebu tuangalie uthibitisho wa maelezo hayo katika Data Na. 6 ifuatayo:

***Data Na. 6:***

…mimi huwa ninawapa wanafunzi kazi za kuandika kuhusu lakabu zao na kuziwasilisha darasani. … unakuta sarufi aliyoitumia mwanafunzi mmoja kuelezea lakabu yake ni tofauti na sarufi aliyoitumia mwanafunzi mwingine. Pia, baadhi ya wanafunzi wanakosea kutumia sarufi, hivyo mimi hulazimika kufundisha sarufi zote zilizojitokeza katika kazi hizo ili kila mwanafunzi aelewe. Nimeona kuwa wanafunzi wengi wanajifunza sarufi hiyo kwa uzingativu mkubwa ili waweze kuandika kazi zao kwa usahihi. Kwa hiyo, ninapofundisha sarufi iliyojitokeza katika uwasilishaji hujikuta ninafundisha vipengele mbalimbali vya sarufi kwa muda mfupi na kwa urahisi kwa sababu kila mwanafunzi anataka kuielewa sarufi iliyomshinda na sarufi mpya iliyojitokeza.

Kwa kurejelea matokeo katika Nukuu Na. 5 na Na. 6, imebainika kuwa kwa baadhi ya walimu matumizi ya lakabu za wanafunzi yanarahisisha ufundishaji wa sarufi pasipo kufahamu kuwa ni mbinu au mkakati unaofaa kutumia kufundishia sarufi. Hawa ni walimu ambao husahihisha makosa ya kisarufi na kufundisha sarufi mpya inayojitokeza wakati wa umwasilishaji kazi za wanafunzi kuhusu historia za lakabu zao. Kwa upande mwingine, makala hii inaonesha kuwa walimu wengine wanatumia lakabu za wanafunzi wakifahamu kuwa ni mbinu ya kufundishia vipengele vya sarufi kama vile kuunda lakabu na kazi za viambishi.

Hata hivyo, walimu wanaofundisha vipengele tajwa vya sarufi wakifahamu kuwa ni mbinu au mikakati ya kurahisisha ufundishaji wa sarufi na walimu waliosahihisha vipengele vya sarufi mpya na kusahihisha sarufi iliyokosewa wakati wa uwasilishaji wa kazi za wanafunzi kuhusu lakabu zao, wamefanikiwa kufundisha sarufi kirahisi. Matokeo hayo yanaonesha kuwa matumizi ya lakabu za wanafunzi yana mchango katika kurahisisha ufundishaji wa sarufi pasipo kujali kama watumiaji wa lakabu hizo wanafahamu au hawafahamu kuwa lakabu za wanafunzi ni mkakati unaoweza kutumiwa kurahisisha ufundishaji wa sarufi. Hivyo, licha ya lakabu kutotambulika kama mbinu ya ufundishaji wa Lgn, zinafaa kutumika kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn.

Pia, ingawa makala hii haikumakinikia ongezeko la walimu wanaotumia lakabu kufundishia Kiswahili kama Lgn lakini kauli iliyotolewa katika Data Na. 4 kuwa kwa sasa idadi ya walimu wanaotumia lakabu za wanafunzi kufundisha sarufi inaongezeka, inaibua jambo la kulimakinikia ili kuhakikisha kuwa walimu wanaohamasika kutumia lakabu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn wana maarifa ya kutumia lakabu hizo kwa namna inayorahisisha ufundishaji. Ikiwa walimu wanaohamasika kutumia lakabu hawana maarifa kuhusu namna lakabu zinavyorahisisha ufundishaji wa Kiswahili, hali hiyo inafaa ishughulikiwe kwa kuwapa walimu maarifa yanayohusiana na namna ya kutumia lakabu za wanafunzi kurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn. Walimu wakipata mafunzo hayo wataendana na maelezo ya MEK yanayosisitiza kuwa na walimu wanaoweza kuyatumia mazingira ya ujifunzaji kwa namna inayowasaidia wanafunzi kufanikiwa kujifunza Lgn. Pia, walimu hao wakipata maarifa hayo wataongeza ubunifu wa kutumia mikakati au mitindo mipya ya kufundishia Kiswahili kama Lgn hususani kipengele cha sarufi (Saleh, 2019).

### 4.2 Matumizi ya Lakabu Kama Mkakati wa Kurahisisha Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn

Kwa upande mwingine, makala hii imebaini kuwa baadhi ya wanafunzi hutumia lakabu kama mkakati wa kurahisisha ujifunzaji. MEK ya Gardner 2005 imeonesha kuwa mikakati mbalimbali hutumiwa na wanafunzi wenye motisha ya ujifunzaji wa lugha ya pili/kigeni ili kupata mafanikio ya juu katika ujifunzaji wa lugha lengwa. Maelezo hayo yanalandana na maelezo ya Fatawi (2019) na Saleh (2019) ambao wanakubaliana kuwa wajifunzaji wa Lgn hutumia mikakati mbalimbali ili kurahisisha ujifunzaji. Hata hivyo, Saleh (2019) anaeleza kuwa wajifunzaji wa Lgn wanatofautiana katika ujifunzaji, hivyo, hutumia mikakati na mitindo tofauti ya ujifunzaji. Mutenyo na wenzake (2021) wanaitazama mitindo ya ujifunzaji wa lugha kama mielekeo ya jumla ambayo mjifunzaji wa lugha hutumia wakati wa ujifunzaji wa lugha ya mawasiliano. Kwa hiyo, katika makala hii istilahi za mitindo na mikakati ya ujifunzaji zinarejelea kitu kimoja. Kutokana na mahojiano yaliyofanyika, wanafunzi walitumia mikakati tofautitofauti kulingana na tofauti zao za kiujifunzaji. Katika makala hii mikakati iliyotumiwa na baadhi ya wanafunzi katika kurahisisha ujifunzaji ni kama kujifunza kwa kusikiliza muziki unaohusu lakabu, kutafuta maana za lakabu, kuandika sentensi kuhusu lakabu na kuandika historia

ya lakabu. Mikakati hiyo imefafanuliwa kama ifuatavyo:

**4.2.1 Kujifunza kwa Kusikiliza Muziki Unaohusu Lakabu**

Usikilizaji wa muziki unabainishwa kama moja ya mikakati inayorahisisha ujifunzaji wa Lgn (Fatawi, 2019; Makame, 2020). Lakini miziki inayohusishwa na kurahisisha ujifunzaji wa Lgn katika makala hii inahusiana na lakabu za wanafunzi. Maelezo ya Atolagbe (2015) yanaonesha kuwa wanafunzi hutumia lakabu kwa namna ya kibunifu kujifunza vipengele mbalimbali vya lugha. Aidha, Mapunda (2014) na Sobane (2016) wanakubaliana na maelezo ya Atolagbe wakieleza kuwa baadhi ya lakabu hutumiwa na wanafunzi kujikumbusha dhana mbalimbali. Makala hii imebaini kuwa baadhi ya wanafunzi walitumia miziki ya Kiswahili inayohusiana na lakabu zao kama mkakati wa kujifunza Kiswahili kama Lgn. Kwa mfano, mwanafunzi aliyepewa lakabu ya *Zuena* alijifunza Kiswahili kupitia muziki uitwao 'Zuena Mtoto Aliyeumbika' kwa sababu lakabu yake ilitokana na kuupenda muziki huo. Ufafanuzi zaidi ulionesha kuwa muziki huo ulimpa mwanafunzi mafanikio ya kujifunza Kiswahili kama Lgn kwa sababu alijifunza maneno mapya ya Kiswahili katika muziki huo. Maneno mapya ni yale ambayo wanafunzi wanakutana nayo kwa mara ya kwanza ambayo hawafahamu maana yake (Makame, 2020). Aidha, maelezo ya mtoataarifa ambaye ni mwalimu yaliongeza kuwa wanafunzi waliojifunza Kiswahili kwa kutumia mkakati wa kusikiliza miziki ya Kiswahili walifanikiwa kujifunza Kiswahili na kuimarisha stadi za kusikiliza na kuzungumza. Hali hiyo inaonesha kuwa lakabu za wanafunzi zina mchango katika kuchochea matumizi ya mikakati inayotokana na motisha ya ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Kutokana na matokeo hayo, matumizi ya lakabu za wanafunzi yanapochochea motisha ya ujifunzaji wa Kiswahili yanaibua ubunifu wa kujifunza Kiswahili kama vile ubunifu wa kutumia muziki kama mkakati wa kujifunza Kiswahili kama Lgn. Mkakati huo umebainika kuwa unarahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn.

Katika utafiti uliofanywa na Mutenyo na wenzake (2021) nchini Uganda mtindo wa kusiskiliza muziki wa Kiswahili ulibainika kutumika na wafanyabiashara waliojifunza Kiswahili kama lugha ya biashara na ulirahisisha ujifunzaji huo.Ingawa utafiti huo haukushughulikia matumizi ya lakabu lakini umeonesha kuwa kusikiliza muziki wa Kiswahili kunarahisisha ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Pia, licha ya makala hii kutokubainisha ni kwa kiasi gani wanafunzi walitafuta maana za maneno yaliyotumika katika muziki waliosikiliza lakini walitumia mkakati huo kurahisisha ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Pia, mkakati huo uliwawezesha wanafunzi kuimarisha stadi za kusikiliza na kuzungumza. Hali hiyo inaonesha kuwa mkakati wa kusiskiliza muziki unarahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kwa namna mbalimbali.

**4.2.2 Ujifunzaji wa Maneno Mapya ya Kiswahili kwa Kutumia Lakabu**

Maneno mapya ni yale ambayo mwanafunzi anakutana nayo kwa mara ya kwanza na haelewi maana yake (Makame, 2020). Makala hii imebaini kuwa matumizi ya lakabu huwarahisishia wanafunzi kujifunza maneno mapya ya Kiswahili kwa namna mbili. Kwanza, wanafunzi hujifunza maneno mapya ya Kiswahili kwa kutafuta maana za lakabu. Wakati wa kufanya usaili kuhusu namna lakabu zinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn, katika maelezo ya watoataarifa ambao ni wanafunzi, ilibainika kuwa baadhi ya wanafunzi walitafuta maana za lakabu za wanafunzi wengine kutoka kwa walimu, wanafunzi na kwa kusoma katika kamusi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alieleza jinsi alivyojifunza Kiswahili kwa kutafuta maana za lakabu za wanafunzi wengine wakati akijifunza Kiswahili nchini China kama inavyodhihirika katika Data Na. 7 ifuatayo:

***Data Na. 7:***

…wakati ninajifunza Kiswahili pale China nilijifunza maana za majina ya wanafunzi 22 katika madarasa mengine na hapa Tanzania ninaendelea kujifunza maana za majina ya wanafunzi wengine.

Data Na. 7 hapo juu inabainisha namna wanafunzi wanavyojifunza Lgn kupitia lakabu za wanafunzi wenzao.

Pia, watoataarifa wengine ambao ni walimu waliongeza maelezo kuhusu namna wanafunzi wanavyotumia lakabu kurahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Walimu wawili walieleza kuwa, wapo wanafunzi wadadisi ambao hutafuta maana za lakabu za wanafunzi wengine ama kwa kuuliza au kwa kusoma. Naye mwalimu mwingine katika Data Na. 8 ifuatayo anatoa ufafanuzi zaidi kuhusu mchango wa maana za lakabu katika kurahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn.

***Data Na. 8:***

…faida moja kubwa ya kutumia lakabu za wanafunzi ni kurahisisha kujifunza Kiswahili… kwa kipindi ambacho nimefundisha katika kituo hiki nimekuwa nikifuatwa na wanafunzi wakiwa na lakabu za wanafunzi wenzao wakitaka niwaeleze maana za lakabu hizo… ingawa walimu wengi hawajui lakini ninafikiri hii inaweza kuwa ni mbinu nzuri sana ya kurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni hapa Tanzania… kwa mfano, ukimpa kila mwanafunzi lakabu tano za wanafunzi wa miaka iliyopita ukawaambia watafute maana zake ninadhani watakuwa wamejifunza Kiswahili kwa namna rahisi…

Kwa kurejelea Data Na. 7 na Data Na. 8, inaonekana kuwa baadhi ya wanafunzi walijifunza maneno mapya ya Kiswahili kwa kutafuta maana za lakabu zao na lakabu za wanafunzi wengine kwa

kuwauliza walimu, wanafunzi wenye lakabu na kwa kusoma katika kamusi. Fatawi (2019) anasisitiza matumizi ya mikakati binafsi katika ujifunzaji wa Lgn akieleza kuwa mikakati hiyo ina faida kama vile kuchochea ubunifu, motisha na kurahisisha ujifunzaji. Aidha, maelezo hayo hayatofautiani na maelezo ya Gardner (2005) katika MEK ambayo yanaonesha kuwa mjifunzaji wa Lgn mwenye malengo ya kufanikiwa kujifunza lugha hiyo hutumia mikakati mbalimbali ya ujifunzaji. Atolagbe na wenzake (2015) nao wana mawazo sawa na wataalamu waliotangulia wakieleza kuwa wanafunzi hutumia lakabu zao kwa namna ya kuonesha ubunifu katika kujifunza vipengele mbalimbali vya lugha. Maelezo ya wataalamu hao na matokeo katika makala hii yanadhihirisha kuwa utafutaji wa maana za lakabu ni miongoni mwa mikakati binafsi ya wanafunzi inayoweza kutumiwa kurahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn kutokana na kuzitumia lakabu hizo kibunifu. Hii ni kwa sababu matokeo yameonesha namna wanafunzi walivyozitumia lakabu kujifunza maneno ya mapya ya Kiswahili kwa kutafuta maana za lakabu kutoka katika vyanzo mbalimbali.

Pili, makala hii imebaini kuwa wanafunzi hujifunza maneno mapya ya Kiswahili walimu wanapowapa lakabu na kuwaeleza maana zake. Katika matokeo yaliyopatikana, walimu 04 walieleza kuwa hueleza maana ya lakabu kabla wanafunzi hawajapewa lakabu hizo. Kama inavyoeleweka, lugha ni maneno na lakabu ni sehemu ya maneno ya lugha ya Kiswahili. Hivyo, wanafunzi wanapoelezwa maana za lakabu na kupata maneno mapya, wanakuwa wamejifunza lugha ya Kiswahili kirahisi hususani kipengele cha sarufi maana. Licha ya urahisi huo, walimu hawawaelezi wanafunzi maana za lakabu kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn bali wanaeleza maana za lakabu za wanafunzi kwa kuwa ni utaratibu wa kawaida wa kuwaeleza wanafunzi maana ya lakabu zao kabla ya kuwapa lakabu husika.

Kulingana na matokeo hayo walimu waliotumia lakabu kufundisha maneno mapya walifanikiwa fundisha Kiswahili kwa namna rahisi. Pia, wanafunzi waliojifunza Kiswahili kwa kutafuta maana za lakabu walifanikiwa kujifunza maneno mapya mengi ya Kiswahili. Hali hiyo inaonesha kuwa upo umuhimu wa kufanya mambo mawili yatakayochangia kurahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kwa kujifunza maneno mapya kutokana na maana za lakabu. Kwanza, ni kuwapa walimu maarifa kuhusu namna wanavyoweza kutumia lakabu za wanafunzi kurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kwa kueleza maana za lakabu mbalimbali. Ikiwa walimu watapatiwa mafunzo hayo, kutakuwa na ongezeko la walimu wenye maarifa kuhusu namna mbalimbali za kutumia lakabu za wanafunzi kurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn. Walimu wakiwa na maarifa hayo, yatawasaidia kufundisha Kiswahili kirahisi kama ilivyobainika kwa baadhi ya walimu. Vilevile, ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni utaendelea kuwa rahisi kutokana na kuongezeka kwa mbinu mpya ya ufundishaji na ujifunzaji wake. Aidha, ufundishaji utakuwa rahisi zaidi kwa sababu ni mbinu ambayo wakati mwingine walimu wanaitumia kulingana na mahitaji ya wanafunzi na si kulingana na mtaala wa ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Pili, ni kuwaelimisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa utafutaji wa maana za lakabu katika kurahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Wanafunzi wakipatiwa maarifa hayo kutakuwa na ongezeko la wanafunzi wenye maarifa yanayorahisisha kujifunza Kiswahili kama Lgn.

### 4.2.3 Uandishi wa Sentensi Zinazohusu Lakabu

Mkakati mwingine unaorahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn ni kujifunza Kiswahili kwa kuandika sentensi zinazohusiana na lakabu za wanafunzi. Wakati watoataarifa walimu wanahojiwa kuhusu faida za kutumia lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji, yalipatikana majibu yafuatayo kama Data Na. 9 na Data Na. 10 zinavyoonesha.

***Data Na. 9:***

…wanafunzi wangu wawili walikuwa na mkakati wa kuandika sentensi zinazohusiana na lakabu zao mara kwa mara na kuwapa walimu tofautitofauti kuwasahihishia. Wakati ninawasahihishia kazi waliyoandika kuhusu lakabu zao walinihakikishia kuwa watakuwa na mafanikio ya juu katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa kutumia mkakati huo ifikapo mwisho wa programu yao…na ndivyo ilivyokuwa.

***Data Na. 10:***

…niliwahi kuwa na wanafunzi wawili ambao walipenda sana kuandika insha na kunipa niwasahihishie. Wanafunzi hao walianza kuandika insha kuhusu lakabu zao na baadaye waliendelea kuandika isha kuhusu vitu vingine na kuendelea kunipa niwasahihishie… wanafunzi hao walidhamiria kujifunza Kiswahili kinachoendana na lakabu zao….kwa mfano, *Almasi* alitumia mkakati huo na alikuwa mwanafunzi bora hapa kituoni kwetu kwa wastani wa asilimia 98 na *Zawadi* alikuwa mwanafunzi bora aliporudi katika Chuo Kikuu cha Michigan …moja ya mambo yaliyochangia mafanikio hayo ni motisha ya lakabu zao. Moja ya mikakati waliyoitumia kama sehemu ya motisha yao ni mkakati wa kuandika insha mbalimbali ili watetee lakabu zao.

Data Na. 9 na Data Na. 10 hapo juu zinabainisha mbinu ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn inayohusiana na uandishi wa sentensi zinazohusu lakabu za wanafunzi. Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walikuwa na majibu yanayofanana na majibu yaliyotolewa na walimu. Mwanafunzi mmoja mtoataarifa aliyeitwa *Zawadi* alieleza kuwa wakati anajifunza Kiswahili aliandika sentensi nyingi kuhusu lakabu yake. Maelezo ya mwanafunzi yalionesha kuwa mkakati wa kuandika

sentensi ulikuwa miongoni mwa mambo yaliyomfanikisha kujifunza Kiswahili kwa kiwango cha juu kwa sababu walimu walimsaidia kuboresha sarufi yake kiasi cha kufikia kuwa mwanafunzi bora katika somo la Kiswahili. Aidha, *Almasi* ambaye pia aliandika sentensi nyingi katika, insha iliyohusu lakabu yake na insha kuhusu vitu vingine alikuwa mwanafunzi bora katika chuo alichojifunza Kiswahili nchini Tanzania. Mwalimu mmoja alithibitisha hali hiyo akieleza kuwa katika programu ya mwaka 2017 mwanafunzi aliyeitwa *Almasi* ndiye aliyeongoza katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa kufanya vizuri katika stadi za kusikiliza, kuzungumza, kuandika na kusoma. Mwalimu aliongeza kuwa moja ya mbinu zilizomfanikisha *Almasi* kujifunza Kiswahili ni kuandika insha na sentensi mbalimbali ikiwamo kuandika kuhusu lakabu yake.

Sambamba na mafanikio hayo, *Kamusi* na *Mashaka* nao walieleza kuwa walitumia mkakati wa kuandika sentensi kuhusu lakabu zao na kufanikiwa kujifunza Kiswahili kwa kiwango cha juu. Pia, *Mashaka* alieleza kuwa aliandika sentensi thelathini kila siku akizihusisha na lakabu yake na kuhakikisha zinasahihishwa na walimu tofautitofauti. Katika ufafanuzi wake alieleza kuwa aliamua kutumia mkakati wa kutumia jina lake kujifunza Kiswahili ili aondoe mashaka ya kutumia maneno ya Kiswahili ambayo mwanzoni yalimpa hofu ya kuzungumza Kiswahili kwa sababu baadhi yake yalikuwa na maana zaidi ya moja. Naye mwanafunzi aliyejiita *Kamusi* alieleza kuwa kila wiki aliandika sentensi mia moja na kuwapa walimu tofautitofauti wamsahihishie kwa lengo la kufanikiwa kujifunza Kiswahili kinachoendana na lakabu yake ili awe kamusi ya darasa.

Maelezo ya watoataarifa hao yanaonesha kuwa mkakati wa kuandika insha na santensi zinazohusiana na lakabu za wanafunzi ulirahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, lakabu zinawafanya wanafunzi kwenda mbele zaidi na kuandika si tu kuhusu lakabu zao bali kuhusu vitu vingine. Pia, mkakati huo uliwawezesha wanafunzi kuboresha sarufi kwa kuongeza msamiati wa Kiswahili na kuimarisha stadi za kusikiliza, kuzungumza, kuandika na kusoma. Hali hiyo inaonekana kuwa iliwawezesha wanafunzi kufanikiwa kujifunza Kiswahili kama Lgn kwa kiwango cha juu na kuchangia baadhi yao kuwa wanafunzi bora katika ujifunzaji wa Kiswahili nchini Tanzania na katika vyuo vikuu walivyotoka.

MEK imesisitiza kuwa moja ya mambo yanayodhihirisha kwa wajifunzaji wa Lgn wana motisha ya kujifunza ni matumizi ya mikakati inayorahisisha ujifunzaji pamoja na kuwa na malengo ya ujifunzaji ambavyo kwa pamoja hurahisisha ujifunzaji. Hivyo basi, ikiwa mkakati huo utatumiwa kama mbinu ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn, utawarahisishia walimu kufundisha na wanafunzi kujifunza. Hii ni kwa sababu matokeo ya utafiti yameonesha kuwa wanafunzi waliotumia mkakati huo kujifunza Kiswahili kama Lgn walipata mafanikio ya juu katika ujifunzaji kwa sababu lakabu zao zimekuwa motisha ya kutumia mkakati huo. Hivyo, ili kurahisisha ujifunzaji, ni muhimu kwa walimu wanaofundisha Kiswahili kama Lgn katika vyuo vinavyofundisha lugha hiyo nchini Tanzania wauchukulie mkakati huo kama mbinu mojawapo ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania.

### 4.2.4 Uandishi wa Historia Kuhusu Lakabu

Lakabu huambatana na kubeba maarifa mbalimbali yanayohusiana na mwenye lakabu husika (Filani na Melefa, 2014). Miongoni mwa maarifa yanayobebwa na lakabu za watu yanahusu historia za maisha yao (Laslie na Skipper, 1990; Mapako, 2015; Garayeva na wenzake, 2016). Katika kubainisha namna lakabu zinavyotumika kama mkakati wa kurahisisha ujifunzaji wa Kiswahili, baadhi ya wanafunzi walijifunza Kiswahili kwa kuchunguza na kuandika historia za lakabu zao na kuziwasilisha darasani. Kwa mfano, mwanafunzi aliyapewa lakabu ya *Juma* aliamua kuchunguza na kuandika historia ya jina hilo kisha akaiwasilisha darasani. Mwanafunzi mwingine aliyeitwa *Kiboko* alichunguza kuhusu maisha ya mnyama aitwaye kiboko na kuwasilisha darasani. Pia, mwanafunzi aliyeitwa *Tembo* aliandika historia ya mnyama tembo ambaye ndiye mwenye jina alilopewa.

Maelezo mengine yaliyotolewa na watoataarifa ambao ni walimu yalionesha kuwa baadhi ya walimu waliwapa wanafunzi kazi ya kuandika historia za lakabu zao. Maelezo ya walimu yalikuwa kama ifuatavyo:

***Data Na. 11:***

…nilikuwa na mwanafunzi anaitwa *Mjakaranda* nikampa kazi ya kuandika kuhusu mti wa mjakaranda na sifa zake ili aje awasilishe darasani….unajua mwanafunzi anapotoka nje ya darasa kufanya kazi hiyo anapata fursa ya kuongea na watu hivyo anajifunza Kiswahili na anaimarisha stadi ya kuzungumza, kusikiliza na kuandika na kusoma…

***Data Na. 12:***

…niliwahi kuwapa wanafunzi wawili kazi ya kuandika kuhusu lakabu zao, wanafunzi hao waliitwa *Tembo* na mwingine *Tausi*. …sikuwahi kufahamu kuwa tembo ndiye mnyama anayebeba mimba kwa muda mrefu kuliko wanyama wote. Pia, sikufahamu kuwa tembo ni miongoni mwa wanyama wenye kumbukumbu zaidi ya wengine wala sikufahamu kuwa ana tabia ya kulipiza kisasi kuliko wanyama wote, lakini historia ya mwanafunzi ilinifundisha yote hayo. Pia, *Tausi* aliandika historia nzuri kuhusu ndege huyo…kitu cha msingi hakikuwa kupata historia bali wanafunzi wapate fursa ya kujifunza Kiswahili…. wanafunzi hao walijifunza mambo mengi kuhusu lugha ya Kiswahili…

Matokeo katika Data Na. 11 na Data Na. 12 yanaonesha kuwa wanafunzi waliandika historia kuhusu lakabu zao na kuwasilisha darasani. Baadhi ya wanafunzi waliamua wenyewe kuandika historia kuhusu lakabu zao huku wengine wakipewa maelekezo na walimu ya kuandika kuhusu lakabu hizo. Kama inavyoonekana katika maelezo katika Data Na. 11 na Data Na. 12 lengo la kuandika historia za lakabu halikuwa kupata historia za lakabu bali kujifunza Kiswahili. Hali hiyo imethibitika kuwa wanafunzi walijifunza sarufi, waliimarisha stadi za kuzungumza, kusikiliza, kuandika na kusoma. Aidha, licha ya kutodhamiria kupata historia za lakabu walimu na wanafunzi walipata maarifa ya ziada yanaohusiana na historia za wanyama ambao majina yao yalitumika kama lakabu za wanafunzi.

Kutokana na matokeo yanayohusu motisha ya ujifunzaji, matumizi ya lakabu za wanafunzi yanachangia wanafunzi kuwa na motisha tofautitofauti zinazorahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Aidha, matumizi ya lakabu za wanafunzi yanachochea wanafunzi kuwa na motisha inayoibua ubunifu wa kutumia mikakati inayorahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Kauli hiyo inadhihirisha kuwa matumizi ya lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn ni muhimu kwa sababu yanachangia ubunifu wa kutumia mitindo mbalimbali ya ujifunzaji. Pia, matumizi ya mikakati mbalimbali ni muhimu katika ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn.

MEK imeeleza kuwa mjifunzaji wa Lgn mwenye motisha ya ujifunzaji hutumia pia mikakati ya kutimiza malengo yake ya ujifunzaji. Pia, Fatawi (2019) anaeleza kuwa wajifunzaji wa Lgn wanapotumia mikakati binafsi ya ujifunzaji mikakati hiyo hurahisisha ujifunzaji. Hivyo, kama mkakati wa kuandika historia za lakabu utatumika kama mbinu ya ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn itakuwa ni miongoni mwa mbinu zinazorahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Hii ni kwa sababu mkakati huo uliwarahisishia baadhi ya wanafunzi kujifunza vipengele muhimu vya lugha ya Kiswahili kama vile sarufi, maneno mapya na stadi za lugha. Hali hiyo inadhihirisha kuwa mkakati wa kuandika historia za lakabu unafaa kutumika kama mbinu mojawapo ya ufundishaji wa Lgn.

Hivyo basi, lakabu za wanafunzi zikiendelea kutumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn, wanafunzi watapata motisha ya kujifunza zaidi. Pia, wanafunzi watakuwa wabunifu zaidi wa kutumia lakabu katika ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Hii ni kwa sababu mitindo ya mjifunzaji L2/Lgn huhusisha mitindo binafsi ya kumwezesha kujifunza namna ya kuitumia mitindo mipya katika kurahisisha ujifunzaji. Hata hivyo, ili kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn, ni muhimu kuchukua tahadhari wakati wa kutumia mitindo na mikakati mipya ya ufundishaji na ujifunzaji wa Lgn.

## 4.3 HITIMISHO

Makala hii imebaini kuwa lakabu za wanafunzi hutumiwa na walimu na wanafunzi kwa namna mbalimbali kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Katika matumizi hayo baadhi ya walimu wamekuwa wakitumia lakabu kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kama Lgn kwa kuwafundisha wanafunzi kulingana na tabia na uwezo wao wa ujifunzaji unaobainishwa na lakabu zao. Pia, walimu hutumia lakabu za wanafunzi kurahisisha ufundishaji wa sarufi. Walimu hao wamegawanyika katika makundi mawili, kundi la kwanza ni walimu wenye maarifa kuwa lakabu ni mbinu inayofaa kufundishia sarufi. Walimu hao hutumia lakabu kufundisha vipengele vya sarufi kama vile miundo ya lakabu na kazi za viambishi. Kundi la pili, ni walimu ambao hawana maarifa kuwa lakabu ni mbinu ya kufundishia sarufi lakini kutokana na kazi wanazowapa wanafunzi waandike kuhusu lakabu zao hujikuta wamefundisha sarufi kwa njia rahisi pasipo hata kufuata mtaala wa ufundishaji. Hawa ni walimu ambao baada ya kuwapa wanafunzi kazi hizo wakati wa uwasilishaji hunukuu sarufi mpya na sarufi iliyokosewa kisha baadaye hufundisha sarufi hiyo. Aidha, wanafunzi nao wanazitumia lakabu kama mkakati wa kurahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn kwa namna mbalimbali kama vile kujifunza kwa kusikiliza muziki wa Kiswahili unaohusiana na lakabu na miziki mingine inayohusiana na lakabu, kutafuta maana za lakabu mbalimbali, kuandika sentensi kuhusu lakabu zao na kujifunza Kiswahili kupitia uandishi wa historia za lakabu zao.

Kwa kuwa walimu na wanafunzi wenye maarifa kuhusu matumizi ya lakabu kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn ni asilimia ndogo, makala hii inapendekeza mambo mawili. Kwanza, walimu wapewe mafunzo kuhusu namna lakabu zinavyoweza kutumiwa kama mkakati wa kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Pili, wanafunzi waelimishwe kuhusu namna ambavyo matumizi ya lakabu yanarahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Pia, makala hii inapendekeza kufanyika tafiti kuhusu athari za kutumia lakabu za wanafunzi katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Aidha, utafiti ufanyike kuchunguza ni kwa nini lakabu za wanafunzi ndizo zinatumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni nchini Tanzania.

## 4.5 MAREJELEO


- Afful, J. B. A. (2007). "Address Terms and Variation among University Students in Ghana". *Nordic Journal of African Studies*, Juz, *16*(2), 179-196.
- Atolagbe, D., Abegunde, C., & Morofonfoye, O. (2015). Generation and attribution of nicknames

among secondary school students: Indices of linguistic creativity. *Research on Humanities and Social Sciences*, *5*(20), 104-109.

- Bobrova, M. V. (2022). Nicknames in teaching Russian as a foreign language. *Russian Language Studies*, *20*(1), 22-34.
- De Klerk, V., & Bosch, B. (1997). The sound patterns of English nicknames. *Language Sciences*, *19*(4), 289-301.
- Diao, W. (2014). Between Ethnic and English Names: Name Choice for Transnational Chinese Students in a US Academic Community. *Journal of International Students*, *4*(3), 205-222.
- Fatawi, Z. M. (2019). *Mikakati Binafsi ya Kujifunza Lugha Inayomsaidia Mwanafunzi wa Kigeni Kuzungumza Lugha ya Kiswahili*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Elimu Katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wazungumzaji wa Lugha Nyingine (M.Ed TEKSOL) (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.
- Filani, I., & Melefa, O. M. (2014). A socio-semiotic study of nicknaming among undergraduates in a Nigerian University. *Linguistik online*, *68*(6), 21-42.
- Garayeva, A. K., Akhmetzyanov, I. G., & Khismatullina, L. G. (2016). The Significance of Learning Nicknames of Public Figures in Modern English and American Language Models of the World. *International Journal of Environmental and Science Education*, *11*(17), 10337-10345.
- Koehn, S. C. (2015). "Use of Self-selected Nicknames by Female Kuwaiti Students and their Perception of the Impact of Nicknames up on their Learning in the Classroom". *Near and Middle Eastern Journal of Research in Education*. Inapatikana katika http://dx.doi.org/10.5339/nmejre.2015.2. Ilisomwa tarehe 21 Januari 2022.
- Lakaw, A. (2006). *Hiding Behind Nicknames: A Linguistc Study of Anonymity in IRC Chatrooms*. Vaxjo University. Inapatikana katika http://Inu.diva-portal.org/smash/record.jsf?pid=diva2:206935. Ilisomwa tarehe 11 Februari 2023.
- Leslie, P. L., & Skipper, J. K. (1990). Toward a theory of nicknames: A case for socio-onomastics. *Names*, *38*(4), 273-282.
- Makame, K. O. (2020). *Utekelezaji wa Mkabala wa Kimawasiliano katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni Nchini Tanzania*. Tazmili ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mapako, F. P. (2015). "A Survey of University Students' Views on the Nature and Significance of Nicknames to the Shona People of Zimbabwe". *Journal of African Studies and Development*, *Juz, 8*(6), 81-87.
- Mapunda, G. (2014). What Do My Students Call Me? Nicknaming of Lecturers by Students at the University of Dar es Salaam. *Journal of Linguistics and Language in Education*, *8*(1), 90-107.
- McDowell, J. H. (1981). Toward a semiotics of nicknaming the Kamsá example. *Journal of American folklore*, 1-18.
- Mutenyo, A. I., Deborah, N. A. N., & Okal Benard, O. (2021), Mitindo ya Ujifunzaji Lugha ya Pili katika Kufanikisha Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Biashara Jijini Kampala, Uganda. *East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature, Juz, 4*(6). Inapatikana katika DOl: 10. 36349/easjehl.2021.v04i06.003. Ilisomwa tarehe 7 Januari 2022.
- Reyes, M., & Rodriguez, J. (2006). *Teaching English in Mixed-ability Classrooms. Some Teachers' Thoughts on Responding to the Needs of all Learners*. Inapatikana katika www.teaching.english.org.uk.
- Saleh, F. H. (2019). *Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni katika Darasa Mseto la Wingilugha*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.
- Sobane, K. (2016). "The Pragmatics of Nicknames Students Use for their Lecturers". Inapatikana katika https://www.researchgate.net/publication/292149459. Ilisomwa tarehe 21 Januari 2022
- Wa'njogu, K. J. (2008). Ufundishaji wa kiswahili Marekani: maendeleo na changamoto. In *Teaching Kiswahili in America: Progress and challenges] Swahili Forum* (Vol. 15, pp. 121-133).
- Wu, X. (2023). Stories of names: exploring Chinese high school language-other-than-English learners' foreign name (s) usage and its role in multilingual identity construction. *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, 1-15.

**Cite This Article:** Joyce Henock Nyiti & Dkt Adventina Buberwa (2024). Matumizi Ya Lakabu Za Wanafunzi Kama Mkakati Wa Kurahisisha Ufundishaji Na Ujifunzaji Wa Kiswahili Kama Lugha Ya Kigeni Nchini Tanzania. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 7*(11), 381-391.